

KISWAHILI

KAZI YA LIKIZO KIDATO CHA KWANZA

MATUMIZI YA LUGHA ALAMA 60

- 1) Andika nomino mbili katika ngeli ya U – YA. (Alama 2)
- 2) Andika kwa umoja (alama 2)
 - i) Machaka ya waridi hayazai maua meusi
 - ii) Walituandikia nyaraka ndefu.
- 3) Onyesha vihisishi katika sentensi zifuatazo.(alama 2)
 - i) Sawasawa! tutakutana kesho.
 - ii) Nabii Musa! Eti kifaru hula nyama
- 4) Onyesha silabi inayowekewa shadda kwenye maneno haya.(alama 4)
 - (i) Karatasi
 - ii)Samahani
- 5) Akifisha kifungu kifuatacho. (alama 3)

Karibu mgeni akaitikia mwenyeji mbona huingii na mlango u wazi naam stareheni kwenye kiti ahsante wakajibu.
- 6) Sahihisha sentensi zifuatazo. (alama2)
 - i)Hao mandugu wamekosana juu ya pesa.
 - ii) Mtu mwenye anakula mkate ametumana aletewe chai.
- 7) Andika methali inayoafikiana na maelezo haya(alama 2)

Taja ala zinazotumika katika kutamka sauti zifuatazo

 - i)/dh/
 - ii)/gh/

(alama 2
- 8)Tunga sentensi yenye mpangilio huu wa kisarufi. (alama 2 ½)

I + W + T + N + V.
- 9)Tunga sentensi kudhihirisha maana tofauti kati ya
(a) Jozi

(b) Njozi

(alama 2)

10) Kanusha sentensi hii katika wingi

Mgonjwa mwenye kichomi aliyelazwa hospitalini ameaga dunia. (alama 2)

11) Tunga sentensi tatu ukitumia neno papara liwe na sifa hizi. (alama 3)

a) Kielezi

b) Nomino

c) kivumishi

(12) Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia 'o' rejeshi na kiambishi ngeli

(alama 2)

Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo.

(13) Andika sentensi zifuatazo kulingana na maagizo uliyopewa.

i) Tano ondoa tatu matokeo ni mbili (anza: Mbili.....)

(alama 1)

ii) Mwalimu huyu anafunza Kiswahili

(Maliza kwa kiashiria kisisitizi)

(alama 1)

iii) Ng'ombe aliyekuwa nyuma ya ua alichechemea kwa vile aliumia ukwato wake. (andika kwa wingi)

(alama 2)

(14) Tunga sentensi ukitumia kisawe cha neno lifuatalo

(alama 2)

Ndwele

(15) Ainisha sentensi hii

(alama 3)

Aliyenichokoza

(16) Geuza sentensi hizi ziwe katika kauli ya kutendewa

(alama 4)

i) Muktubi amempa mwanafunzi jarida.

ii) Bate alivua samaki wengi.

(17) Tunga sentensi zinazoonyesha matumizi ya vihusishi katika hali zifuatazo (alama 4)

i) Uhusiano wa zaidi ya hayo

ii) Kuonyesha chanzo

(18) Geuza kwa wingi. (alama 2)

(i) Njia hii huenda Kisumu

(ii) Wembe huu utafaa.

(19) Tumia kauli ya kutendesha katika sentensi zifuatazo:. (alama 2)

(i) Mukhwana alikunywa pombe mpaka akalewa sana

(ii) Tafadhali hakikisha Omari ameelimika vizuri

(20) Sahihisha sentensi zifuatazo. (alama2)

i) Hao mandugu wamekosana juu ya pesa.

ii) Mtu mwenye anakula mkate ametumana aletewe chai.

(21) Tunga sentensi kubainisha maana tofauti ya maneno haya; (alama 2)

i) Dalili

ii) Dhalili

(22) Eleza maana ya methali ifuatayo: (alama2)

Akikalia kigoda mtii.

(23) Andika katika udogo

Mwanamke alimuua mbuzi kwa shoka. (alama 2)

(24) Weka shadda katika neno 'barabara' ili kuibua maana tofauti ya neno hilo

i) Barabara (maana)

ii) Barabara (maana)

Bwana mwenyezi, muumba wa ardhi na mbingu, twaja mbele yako asubuhi hii kukuomba uendelee kutulinda na kutumiminia kila kilicho chema. Bariki ibada ya leo na sheshe ya sindikiza ya kina mama tutakayokuwa nayo alasiri. Ninaomba haya machache kwa jina la yesu Kristo mkombozi wetu, Amina.

- (a) Taja muktadha wa makala haya. (alama 2)
- (b) Taja sifa zozote tatu za sajili hii zinazojitokeza katika makala haya. (alama 9)
- (c) Taja sifa zingine za lugha ambazo hazikuhusishwa katika makala haya kwa mujibu wa sajili hii. (alama 9)

FASIHI SIMULIZI ALAMA 20

1. Eleza tofauti ya fasihi simulizi na fasihi andishi. (alama 10)
2. Je, ni sifa gani bainishi zinazohusishwa na fasihi simulizi. (alama 10)

